East African Journal of Swahili Studies, Volume 2, Issue 2, 2020
Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 2, Issue 2, 2020
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Aina ya Nyenzo Katika Ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili Katika Shule za Sekondari Nchini Kenya

*Bakari Osundwa Kassim[1*], Dkt. John Kirimi M'raiji[1] & Luganda Manasseh[1]*

[1] Idara ya Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: osundwabakari@mail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*24 Octoba 2020*

**Istilahi Muhimu**:

*Nyenzo, Fasihi Simulizi, Ufundishaji, Kufundishia, Shule za Sekondari.*

**IKISIRI**

Madhumuni ya makala haya yalikuwa kubaini aina ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari katika Kaunti ya Kakamega nchini Kenya kwa kuangazia madarasa ya mwanzo. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Maendeleo ya Kiutambuzi ya Jean Piaget (1896-1980) iliyoasisiwa mwaka 1954 inayosisitiza umuhimu wa kutangamana na matini husika kwa lengo la kuelewa katika hatua za mwanzo za funzo. Utafiti huu ulitumia muundo wa usoroveya elezi. Idadi lengwa ya utafiti huu ni walimu wa somo la Kiswahili pamoja na wanafunzi wa madarasa ya mwanzo katika shule za sekondari katika Kaunti ndogo ya kati ya Kakamega. Mtafiti alitumia mbinu za usampulishaji za kinasibu na kimakusudi kuteua sampuli ya kutumiwa ambayo ilikuwa theluthi moja ya idadi lengwa. Walimu ishirini na tano (25) ambao ni theluthi moja ya walimu wote wanaofundisha Kiswahili katika madarasa ya mwanzo katika shule za sekondari Kaunti ndogo ya kati ya Kakamega na wanafunzi mia mbili hamsini (250) walishirikishwa na data kukusanywa kwa kutumia miongozo ya uchunzaji, hojaji, mahojiano na uchanganuzi wa nyaraka. Data ziliwasilishwa kwa kutumia maelezo, majedwali, vielelezo na viwango vya kiasilimia. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kwamba, walimu wanatumia aina tatu za nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili lakini hawatilii mkazo nyenzo zinazotokana na hali na mazingira mbalimbali ya mfumo wa kijamii katika kufundisha Fasihi Simulizi ya Kiswahili licha ya kuwepo. Utafiti huu utakuwa muhimu kwa sababu mbali na kuwapa walimu uelewa mpana wa aina ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili, utasaidia katika kutambua hali na mazingira inayopatikana kama nyenzo katika ufundishaji na hivyo kuimarisha juhudi za wadau katika sekta ya elimu katika kuboresha matumizi yake. Utafiti ulipendekeza serikali kutenga sehemu maalumu katika Kaunti ili kuwapa

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

walimu nafasi ya kutangamana na aina tofauti ya nyenzo zinazotokana na mifumo ya kijamii kwa kufundisha Fasihi Simulizi ya Kiswahili kwa kuimarisha na kuhifadhi mazingira ya kijamii kwa lengo la kutumika kama nyenzo.

**APA CITATION**

Kassim, B., M'raiji, J., & Manasseh, L. (2020). Aina ya Nyenzo Katika Ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili Katika Shule za Sekondari Nchini Kenya. *East African Journal of Swahili Studies*, *2*(2), 128-143. https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

**CHICAGO CITATION**

Kassim, Bakari, John M'raiji, and Luganda Manasseh. 2020. "Aina ya Nyenzo Katika Ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili Katika Shule za Sekondari Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies* 2 (2), 128-143. https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227.

**HARVARD CITATION**

Kassim, B., M'raiji, J. and Manasseh, L. (2020) "Aina ya Nyenzo Katika Ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili Katika Shule za Sekondari Nchini Kenya", *East African Journal of Swahili Studies*, 2(2), pp. 128-143. doi: 10.37284/eajss.2.2.227.

**IEEE CITATION**

B. Kassim, J. M'raiji, and L. Manasseh, "Aina ya Nyenzo Katika Ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili Katika Shule za Sekondari Nchini Kenya", *EAJSS*, vol. 2, no. 2, pp. 128-143, Oct. 2020.

**MLA CITATION**

Kassim, Bakari, John M'raiji, and Luganda Manasseh. "Aina ya Nyenzo Katika Ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili Katika Shule za Sekondari Nchini Kenya". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 2, no. 2, Oct. 2020, pp. 128-143, doi:10.37284/eajss.2.2.227.

## UTANGULIZI

Shughuli za ufundishaji zinahusisha hatua mbalimbali kati ya mwalimu na mwanafunzi ambapo ujumbe humfikia mwanafunzi kiurahisi kwa kutumia vifaa mbalimbali vinavyopendekezwa na mtalaa kwenye silabasi. KIE (2006) inafafanua nyenzo kama vichoko vinavyoweza kumsaidia mwalimu kufanikisha ufundishaji wake. Inataja nyenzo kuwa na umuhimu wa kumsaidia mwalimu kurahisisha uwasilishaji wa ujumbe wake pamoja na kusisitiza jambo linalofundishwa. Pia inasisitiza kuwa nyenzo zikitumiwa vizuri humfanya mwanafunzi atekeleze kikamilifu na kupata kuelewa dhana vizuri hata kama dhana hiyo ni ya kidhahania. Kutokana na mabadiliko ya Silabasi ya Kiswahili KIE (2002), nyenzo imepewa nafasi kubwa katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Bennaars, Otiende na Boisvert (1994), wanaeleza kuhusu dhima ya mazingira na kanuni za ufunzaji wa somo na vile humwezesha mwanafunzi kujifunza kwa urahisi na kuelewa mambo mbalimbali yanayohusiana na jamii zao; hali ambayo huwa na taathira kwa mitazamo na mielekeo yao katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Nyenzo katika ufundishaji huzidisha ufanisi na hukuza kiwango cha uhifadhi wa hoja mioyoni au akilini miongoni mwa wanafunzi. Hali hii yawezekana ili wanafunzi watumie hisia zao zote kuona, kuhisi, kunusa na kusikia (Musau & Chacha, 2001).

Mwakyembe (1982) anasisitiza kuwa nyenzo zinaweza kutumiwa kurutubisha njia za kufundishia lugha kama mihadhara, kukariri, majadiliano, masaili na kadhalika. Nyenzo huleta mvuto darasani, huongeza maelezo ya maneno, huleta uasilia, huokoa muda na kadhalika. Kulingana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2004), vipengele vya ufundishaji wa Kiswahili ni kustawisha stadi ya usomaji fasaha, maongezi kwa Kiswahili darasani, maandalizi ya kufunza Kiswahili, nyenzo za kufunzia, masuala ya jinsia katika Kiswahili na kutathminiwa kwa utekelezaji wake. Kulingana na Sifuna (1996), ubora wa elimu katika shule nchini Kenya hutegemea maandalizi na uimarishaji wa walimu. Gathumbi na Ssebbunga (2005) wanasema nyenzo za kufundisha humwathiri mwanafunzi na ziwe na sifa zifuatazo; za kuweza kuvutia, kuingiana vizuri na funzo, ziwe za kukuza umbuji wa mwanafunzi na hatimaye ziweze kuingiana vyema na maisha ya kawaida ya wanafunzi. Pappert (1987) na Donhardt (1987) wanapendekeza kuwa tarakilishi inaweza

kutumika pamoja na Nyenzo nyingine kama vile printa, *DVD* na *CD*. Omstein (1990) anasema vifaa hivi husaidia kielimu kutumia viunga mbali vinavyotumia mitambo ya *satellite*. Kwa mujibu wa Macharia na Wario (1989), nyenzo ni vifaa vyote ambavyo vinaweza kutumiwa na mwalimu na wanafunzi ili kuimarisha ufundishaji darasani. Wakati wa maandalizi na matumizi ya nyenzo, lazima mwalimu awazie jinsi zitakavyoimarisha ufundishaji ili kupunguza changamoto zinazozikumba katika matumizi yake. Omstein (1990) na Quist (2000) wanakubaliana kuwa nyenzo hutia wanafunzi motisha huchangia uelewaji, hutoa tajriba tofauti, huhimiza uhusikaji na hubadilisha mitazamo na mbinu za mwalimu na mwanafunzi kuhusu dhana fulani. Licha ya kuwa na mchango mkubwa katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi katika shule za sekondari nchini Kenya, kumekuwa na hali ya kutoridhisha kuhusiana na matumizi ya vifaa hivi katika jamii ambapo hupatikana katika Kaunti ya Kakamega, Kenya (Chesaina, 2007). Baada ya utafiti huu, mtafiti alikusudia kuwa na mapendekezo muhimu kuhusu aina ya Nyenzo kiujumla.

Utafiti huu ulifanyika katika sehemu ya kati, Kaunti ndogo ya Kakamega ya Kati Kaunti ya Kakamega, Kenya. Eneo hili lilikuwa na walimu sabini na tatu (73) wa Kiswahili. Kaunti ndogo ya Kakamega ya Kati inajumuisha wadi ya Shichirayi upande wa kaskazini, Mahiakalo upande wa magharibi na Shieywe upande wa mashariki. Eneo hili lina shule 27 kulingana na orodha ya shule hizi iliyopatikana katika ofisi ya Elimu ya Kaunti ndogo ya Kakamega ya kati. Kulingana na Luvisia (2003) anaeleza kuwa kufahamu maeneo ya utafiti husaidia katika kumfanya mtafiti akubalike. Singleton (1993) anachangia kuwa eneo linalofaa kwa utafiti ni lile la kufikiwa kwa urahisi na lililokubali mtagusano baina ya mtafiti na watafitiwa.

Utafiti ulifanywa nyanjani kwa kuzingatia kanuni za muundo wa usoroveya-elezi katika kuzua njia na mbinu faafu za kukusanya, kuchambua, kuchanganua pamoja na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Mtafiti alitumia muundo wa usoroveya-elezi kwa sababu ulinuia kumwezesha mtafiti kuelewa hali iliyopo kuhusu matumizi ya aina tofauti za nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili shule za upili nchini Kenya, kuieleza na kufasiri matokeo kwa njia iliyo wazi. Kwa mujibu wa Creswell (2006) muundo huu ni mwafaka kutokana na namna ulivyo katika mfumo wa kijamii kama vile asasi za elimu na uwezo wa kuzua data na takwimu zenye habari za kielimu na zenye manufaa ya wadau katika elimu. Utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo kufafanua data zilizokusanywa.

## NADHARIA INAYOONGOZA MAKALA

Utafiti huu ulielekezwa kwa misingi ya nadharia ya Maendeleo ya Utambuzi ya Jean Piaget aliyeishi Uswizi kati ya miaka 1896 na 1980. Kimsingi, Piaget alikuwa mwana elimuviumbe na falsafa. Msingi huu ulimfanya kuhusika na jinsi ambavyo maarifa hujengwa katika viumbe tofauti ndiposa akashughulika na maendeleo ya kiutambuzi ya mtoto na mazingira yake ambayo yanaweza kuimarisha ujifunzaji. Nadharia hii inaonyesha kuwa kutangamana na hali na mazingira halisia yana mchango mkubwa katika michakato ya upokeaji maarifa kwa mwanafunzi ndiposa utafiti huu ulikusudia kubaini aina ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili kwa kuzingatia mifumo ya kijamii katika maeneo ya Kakamega, Kenya.

Kulingana na Gagne (2006), Piaget alifanya utafiti kuhusu masuala ya kiasilia ambayo yaliathiri jinsi mtoto akuavyo kiutambuzi. Kwa miaka ishirini alifanya utafiti katika shule ya msingi ya Rousseau kule Geneva hasa kwenye madarasa ya mwanzo ya chekechea. Katika utafiti wake alitambua kuwa zipo hatua za kimsingi za maendeleo ya kiutambuzi kutegemea umri wa mwanafunzi kuelewa vyema ajifunzacho iwapo mafunzo yataambatana na matumizi muafaka ya nyenzo. Kwa kuegemea msingi huu wa nadharia ya kuwa umri unaathiri upokeaji wa matini, mtafiti alikusudia kufanya uchunguzi kuhusu aina ya nyenzo inayotumika kwa wingi katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili kwa kuegemea madarasa ya mwanzo katika shule za sekondari ambapo vidato vya kwanza ndivyo vilikuwa kusudiwa kwa sababu ndivyo huwa vya kufanyiwa utangulizi kuhusu ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili.

Piaget alihusika sana na jinsi mawazo ya mtoto hupangika anapoendelea kutagusana na mazingira yake. Huanza kutambua vitu jinsi anavyoendelea

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

kutaguzana navyo Katika mazingira ya ufundishaji kwa kushirikisha nyenzo mwafaka. Ni katika misingi ya kutaka kupata uhalisia wa matumizi ya aina mbalimbali ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika Kaunti ya Kakamega nchini Kenya ilibainishwa kupitia kwa utafiti huu.

Kulingana na nadharia hii, kuna mambo manne ambayo huchangia mabadiliko ya kimawazo ya mtoto. Mojawapo ya mambo haya ni tajriba yake kuhusu vitu katika mazingira yake. Kwa kawaida watoto lazima waone, wasikilize au kwa njia moja au nyingine wahisi vitu ili waviwazie. Nyenzo ndicho chombo cha pekee ambacho kinaweza kuleta athari hizi katika ufundishaji hasa kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Mawazo haya yalitumiwa na mtafiti kuelekeza utafiti wake kwa kuzingatia nyenzo tofauti katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika shule za sekondari Kaunti ya Kakamega nchini Kenya.

Nadharia ya Maendeleo ya Utambuzi ya Piaget (1896-1980) inadai kuwa usimilishaji huu una uhusiano mkubwa na ufundishaji kimchezo. Nyenzo huleta athari kikamilifu kwenye somo la Kiswahili kwa ufundishaji maendeleo ya jumla ya kiutambuzi. Madai haya ni ya kielelezo kwa mtafiti kuhusu utafiti huu kwa kuwa yalisaidia kubaini aina ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika shule za sekondari Kaunti ya Kakamega, Kenya. Cross (1974) anaeleza kuwa, kwa kiasi kikubwa utambuzi wa mwanafunzi lazima ubadilishwe ili kuingiza mafunzo mapya. Hatua hii anaiita ukubalifu. Umbo, rangi na mwendo katika mafunzo huimarisha ukubalifu wa maarifa mapya. Nyenzo huongeza athari hizi kwenye mafunzo. Kwa hivyo, swala la aina ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika shule za sekondari lilichunguzwa kwa misingi ya nadharia hii kwa kuegemea mfumo yote ya kijamii katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili

Nadharia hii inatilia maanani matumizi ya nyenzo ili kufanikisha ufundishaji. Iwapo wanafunzi wanaweza kujiundia maarifa wenyewe, basi ni lazima wapewe uhuru wa kufanya hivyo. Hali hii huhimiza michezo, majaribio, tajriba ya moja kwa moja na kuhisi hali halisi ya mambo tofauti na maagizo na mihadhara. Kauli hii ilisaidia kuelewa ni aina gani ya nyenzo hutumika katika ujifundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika shule za sekondari Kaunti ya Kakamega nchini Kenya. Kwa hivyo nadharia inapendekeza walimu kutumia mazingira ambamo walimu wa shule za sekondari wanastahili kufundisha Fasihi Simulizi ya Kiswahili ili kuzua ubunifu miongoni mwa wanafunzi. Maendeleo ya kiutambuzi ni kigezo muhimu cha kuzingatia wakati wa ufundishaji na maandalizi ya nyenzo. Kwa misingi ya nadharia hii, utafiti ulichunguza aina ya nyenzo na hali na mazingira yapatikanayo shuleni katika matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili.

## UTEUZI WA SAMPULI

Peil (2002) anafafanua uteuzi wa sampuli kama uchanganuzi wa sehemu fulani ya watu au kitu kuwakilisha watu au kitu kizima. Vile vile Kothari (2003) na Mugenda na Mugenda (2003), wanakubaliana na maelezo haya kwa kusema kuwa uteuzi wa sampuli ni muhimu sana katika utafiti kwa sababu ni vigumu mno kuchunguza idadi nzima ya watu inayotakiwa kwa sababu ya wakati, gharama au usumbufu na hivyo watafiti huchagua na kuzingatia idadi fulani ambayo huitwa sampuli ya kutumiwa. Utafiti huu uliwashirikisha walimu 25, ambao ni asilimia 34% ya walimu 73 wa Kiswahili waliokuwepo katika eneo la kati ya Kaunti ya Kakamega kama wapendekezavyo wataalamu wengi mathalan Ogulla (2002), Mugenda na Mugenda (2003) pamoja na Kothari (2003).Wanafunzi 250 walishirikishwa kwenye utafiti. Utabakishaji ulitumiwa ili kuhakikisha kuwa maoni ya watafitiwa yamewasilishwa vilivyo katika utafiti. Walimu 25 waliokuwa wakifundisha Fasihi Simulizi ya Kiswahili ndio walioshirikishwa katika utafiti huu. Orodha ya shule za kutafitiwa ilipatikana katika eneo la kati ya Kaunti ya Kakamega. Shule ziligawika katika makundi matatu kwa misingi ya viwango vya shule, aina ya shule na muundo wa shule ili kupata matokeo yasiyotegemea kiwango kimoja. Uteuzi huu wa sampuli ulinuia kupata matokeo yasiyoegemea upande wowote.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

**AINA ZA NYENZO**

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kubaini aina mbalimbali ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika shule za sekondari katika Kaunti ya Kakamega. Kupitia kwa hojaji na uchunzaji, mtafiti aliweza kuthibitisha uwepo wa nyenzo aina mbalimbali kupitia kwa uhakiki wa maandishi. Katika utafiti huu ilibainika kuwepo kwa aina tatu ya nyenzo: nyenzo za kutazamwa, nyenzo za kusikilizwa na nyenzo za kusikilizwa na kutazamwa. Kulingana na Kothari (2012), anasema kuwa kwa kutumia uchunzaji, mtafiti hutafuta data kwa kushuhudia yeye mwenyewe na wakati mwingine bila kushirikisha watafitiwa.

KIE (2006), Robinson (1980) Okwalo (2012) wamegawa nyenzo katika makundi matatu makuu yanayojumuisha nyenzo za kusikiliza, nyenzo za kutazamwa na nyenzo za kusikilizwa na kutazamwa. Nyenzo za kusikilizwa huboresha mafunzo kwa kusikilizwa, za kutazamwa kupitia kutazamwa na za kusikilizwa na kutazamwa kupitia kwa kusikia sauti pamoja na kutazama picha au michoro. Mfano wa nyenzo za kusikilizwa ni kama vile kanda za sauti, redio, tarakilishi, televisheni, video, wanasarakasi waalikwa, filamu na tepurekoda. Nyenzo zinazotumika kwa kutazamwa ni kama vile vitabu, vibonzo, ubao, michoro, picha, vifaa halisi, magazeti na majarida, maleba, vinyago, mapiku, projekta , majedwali na mazingira na hali. Nyenzo zinazotumika kwa kutazamwa na kusikiliza ni kama vile filamu, televisheni, wanasarakasi, waalikwa na fanani, video, projekta za sauti na tarakilishi. Mgao huu ni muhimu kwa sababu ulimsaidia mtafiti kutambua aina za nyenzo zitumikazo shuleni na hivyo kuwa rahisi kubaini matumizi ya mazingira na hali katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika shule za sekondari Kaunti ya Kakamega, Kenya.

Aina tofauti za nyenzo zinazopatikana shule tofauti kwa minajili ya ufundishaji wa somo la Kiswahili kiujumla ilijulikana kupitia kwa miongozo ya hojaji kwa walimu pamoja na wanafunzi na mwongozo wa usaili kwa mwalimu wa somo la Kiswahili hasa anayefundisha Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Kila mwalimu aliulizwa kuhusu kuwepo kwa aina gani ya nyenzo katika ufundishaji wake wa somo la Kiswahili na matumizi yake katika hojaji aliyopewa. Kwa kila nyenzo iliyotumika mwalimu alionyesha kwa alama ya mkwaju na kudhihirisha ipo ya kutosha, chache au haipo kabisa. Alama za mikwaju zilijumuishwa pamoja na kupata asilia ya utumizi wake na uwepo wake kwa kila shule. Habari zilipatikana kupitia kwa miongozo ya hojaji na mwongozo wa usaili kwa kuzilinganisha ili kuthibitisha uthabiti wake. Matumizi ya ya njia za utafiti kupitia kwa hojaji kwa kutaja nyenzo zilizokuwepo shuleni kwa idadi ya kiujumla shuleni mwake na kisha kueleza ilipatikana kwa utosho au uchache katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili.

**Nyenzo za Kutazamwa**

Picha, nyenzo, michoro na majedwali ni vifaa muhimu sana vya kufundishia somo husika. Vifaa hivi huwa kichocheo cha kuwasisimua watoto wachanga wa Fasihi (Aras, 2012). Maelezo haya yanaungwa mkono na maoni ya Musau na Chacha (2001). Maoni haya yanajikita katika msingi wa Nadharia ya Maendeleo ya Utambuzi ya Jean Piaget (1896-1980) iliyoasisiwa mwaka wa 1954. Msingi wa Nadharia hii unatambua umri kama kipengele cha msingi katika ujifunzaji matini ya kwanza hasa katika utafiti huu tukilenga somo la Fasihi Simulizi ya Kiswahili kwa vidato vya mwanzo katika shule za sekondari nchini Kenya.


Kulingana na Farrant (1980) na Clark na Starr (1986) ubao ni nyenzo kongwe inayopatikana katika ufundishaji wa kisasa. Ubao hutumika kwa malengo tofauti yakiwemo kutandaza picha, kuchora michoro kama vielelezo, kufafanua maelezo kuhusu hoja, kuonyesha filamu, kunakili hoja yenye uzito wakati mwalimu afundishapo darasani. Lakini kwa maoni tofauti ya Waker (1975), Farrant (1980) na Macharia na Wario (1989) wanataja vibonzo na vinyago kama nyenzo muhimu na faafu kwa ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Katika ufafanuzi wao wanapendekeza sarakasi za vinyago vya mikono kama nyenzo mwafaka kwa kufundishia Fasihi Simulizi hasa hadithi na vichekesho. Hali hii huwapa ujasiri kwa wale ambao wana haya kupitia kwa kuwashirikisha moja kwa moja katika utendaji wa hadithi na vichekesho. Projekta itumiwe badala ya ubao ili kuivuta ilhamu na umakini wa wanafunzi. Mwalimu mwenye hana ujuzi wa kuchora ubaoni na kwenye manila atafaidi kikamilifu kwa kutumia projekta kwa kufuatisha

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

nakili karatasi angavu kisha kuitumia projekta kuzipanua ukutani kulingana na Henson (1982).

Uwepo na utumizi wa aina ya nyenzo za kutazamwa zilirekodiwa kwa kutumia miongozo ya hojaji ya walimu pamoja na wanafunzi na mwongozo wa usaili. Kwa kijumla kulikuwa na aina 13 za nyenzo za kutazamwa. Watafitiwa 25 (100%) walionyesha kuwa hutumia ubao kwa ufundishaji wao na ni nyenzo ambayo iliyopatikana kwa wingi kati ya nyenzo zingine za kutazamwa. Vitabu vilifuata ubao katika utumizi wa nyenzo za kutazamwa 23 (92%). Michoro ilikuwa na watafitiwa 15 (60%), picha watafitiwa 14 (56%), tarakilishi watafitiwa 12 (48%), projekta 10 (40%), mazingira watafitiwa 8 (32%), magazeti na majarida watafitiwa 6 (30%), majedwali watafitiwa 5 (20%), vifaa halisi watafitiwa 3 (12%) na mwisho vibonzo, vinyago na mapiku zilikuwa na mtafiti 1 (4%) mtawalia.

Licha kuwa ubao ni Nyenzo kongwe, ilibainika kuwa ilikuwa inatumika kwa wingi kwa asilimia 100% ya walimu waliotafitiwa wa somo la Kiswahili. Hii ni kutokana na madai ya walimu kuwa hauhitaji ujuzi wowote wala maandalizi mengi na imekuwa na mwongozo wake tangu uundaji wa mtaala wa elimu pamoja na silabasi. Vitabu vinafuata katika matumizi yake katika kufundisha somo la Fasihi ya Kiswahili kwa kufafanulia kila hoja inashughulikiwa na mwalimu ndani au nje ya darasa. Hii ni kwa sababu walimu pamoja na wanafunzi walidhihirisha kuwepo kwa idadi ya kutosha ya vitabu vya Fasihi ya Kiswahili vya kibinafsi na pia vya serikali na hivyo kawaka nafasi kubwa ya kutangamana navyo kwa somo la Kiswahili kila mara na hivyo kupendelewa katika matumizi. Matumizi ya mazingira na hali haijapewa kipao mbele katika matumizi yake kupitia kwa asilimia 32% walimu wanane (8) kwa jumla ya walimu 25 waliotafitiwa. Hii ni licha walimu kubaini kuwepo kwa mazingira faafu na kuwa na mchango chanya katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika shule husika nchini Kenya.




Kielelezo Cha 1: Nyenzo za Kutazamwa


**Nyenzo za Kusikilizwa**

Redio ni nyenzo faafu katika ufundishaji Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Kupitia kwayo wanafunzi huweza kuimarisha usikivu na ubunifu ili kujenga mawazo na maelezo. Redio husaidia wanafunzi kurudia sentensi, kujibu maswali jinsi yanavyoulizwa na mwasilishaji Shitohi (1992). Naye Postman (1979) na Dorr (1984), wanaisifia televisheni kama mfumo wa pili wa elimu.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

Wanasema kuwa televisheni ni mtaala maalum kwa jinsi ambavyo ina mvuto mkubwa kwa wanafunzi itumikapo kama nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Kiujumla kulikuwa na nyenzo nane (8) za kusikilizwa. Kutokana na rekodi za miongozo ya hojaji na usaili, watafitiwa 13 (52%) walisema redio inapatikana shuleni ambapo ilitambuliwa kuwa nyenzo iliyopatikana kwa wingi miongoni mwa nyenzo zingine za kusikilizwa, watafitiwa 12 (48%) wanasarakasi ,watafitiwa 11 (44%) walidhihirisha kuwepo kwa nyenzo ya televisheni shuleni mwao, watafitiwa 5 (20%) kanda za utafitiwa, watafitiwa 8 (32%) tarakilishi, watafitiwa 4 (16%) video, filamu na tepurekoda zilikuwa na mtafitiwa mmoja kila moja (3%).

Kwa ujumla nyenzo za kusikilizwa hazikutiliwa maanani katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili licha ya kuwa redio ilionekana kutumika bali kwa nadra kulingana na watafitiwa husika. Asilimia 90% ya nyenzo za kusikilizwa hazikupatikana kwa shuleni na hivyo kudhihirisha tu asilimia 10% ya nyenzo za kufundisha ilipatikana shuleni kwa kusudi la kufundishia Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Sababu iliyotolewa kwa hili ni kuwa vipindi vilivyokadiriwa kwa somo la Kiswahili ni vichache na hali hii ya matumizi ya nyenzo za kusikiliza huhitaji muda mwingi sana ili somo litimize malengo yao. Pia walimu walisema kuwa nyenzo hizi hupatikana kiurahisi miongoni mwa wanafunzi kwa hivyo hawaoni umuhimu wa kutilia mkazo au kuzitumia darasani kwani wanafunzi hutangamana nazo bila uwepo na uelekezi wa mwalimu kwa sababu za ukuaji na uimarikaji wa kiteknolojia katika kila nyanja ya sanaa ya mawasiliano. Kwa hivyo hawakuona umuhimu wa kutilia mkazo au kuzitumia kwani wanafunzi wanahisi kuwa kwa kuhusishwa na nyenzo hizo ni kama njia mojawapo ya kupoteza muda wa kukamilisha silabasi.




Kielelezo Cha 2: Nyenzo za kusikizwa


**Nyenzo za Kutazamwa na Kusikilizwa**

Kulingana na maelezo ya Pappert (1987) na Donhardt (1987) wanasema kuwa nyenzo inayoweza kutekeleza kikamilifu majukumu mengi ya kielimu ni tarakilishi. Wanaendelea kusema kuwa vifaa vya kisasa vinavyotumia *satelite* ni bora sana maoni yanayoungwa mkono na Omstein (1990). Vifaa hivi humwezesha mwalimu na mwanafunzi kuchagua vipindi vya Kimataifa kwa mafunzo yao. Watambaji na watumbuizaji ni nyenzo muhimu za kufundishia Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Hawa ni watu ambao huweza kuelimisha

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

watu kwa njia ya utumbuizaji kwa sarakasi, nyimbo na hadithi. Vile vile waalikwa au mafanani wanaweza kupewa mualiko ili waweze kuwa wanafunzi tajriba nyingine kando na mwalimu wao wa somo la Kiswahili hasa somo la Fasihi Simulizi ya Kiswahili.

Katika mapendekezo ya silabasi ya shule za sekondari kuhusu somo la Kiswahili (KIE, 2002), nyenzo za kutazamwa na kusikilizwa ni mwafaka kwa vipindi vinavyokusudia kujenga stadi za kusikiliza na kutazama. Katika utafiti huu kulikuwa na nyenzo tisa za kusikilizwa na kutazamwa. Nyenzo ambayo ilipatikana kwa wingi katika shule ni televisheni ambayo ilikuwa na watafitiwa 18 (72%) ambayo watafitiwa wengi walidhihirisha kuwa inapatikana shuleni mwao. Ilifuatwa na tamasha za muziki kwa watafitiwa 15 (60%) ambapo wanafunzi walishiriki moja kwa moja katika mashindano ya muziki. Matumizi ya waalikwa ilifuata kwa watafitiwa 14 (56%), matumizi ya projekta kwa watafitiwa 12 (48%), shughuli za kijamii watafitiwa 11 (44%), wanasarakasi watafitiwa 9 (36%), tarakilishi watafitiwa 3 (12%), video watafitiwa 2 (8%) na mwishowe filamu ambayo haikuwa mtafitiwa hata mmoja (0%). Licha ya kuwa 37% ya walimu walidhihirisha matumizi ya nyenzo hizi za kusikilizwa na kutazamwa, nyenzo zilizotambuliwa ilisemekana hazitumiki kikamilifu jinsi zinavyohitajika. Wanafunzi hushirikishwa kutumia nyenzo hizi kama vifaa vya kuwaburudisha na kuwaliwaza wakati wa mapumziko na wakati wa maamkuli bali si kwa madhumuni ya kuwaongezea maarufu kwa somo la Fasihi Simulizi. Wanafunzi hupewa nafasi ya kutumia televisheni kuona taarifa na nyimbo za kujiliwaza kama vile siku ya Jumapili kama njia mojawapo ya kuabudu. Shughuli za kijamii na mazingira haijatiliwa mkazo kama inavyohitajika kwa kila nyenzo licha ya kuwapa nafasi ya kipekee wanafunzi na walimu kutangamana moja kwa moja na matini ya Fasihi Simulizi ya Kiswahili pasipo na kiungo bali katika hali yake ya kiasilia. Ilibainika kuwa mojawapo ya sababu ya kutotumika vyema ni walimu pamoja na wanafunzi wako na dhana kuwa haiwezi kuwafaidi katika matumizi yake kwani ni mambo ya kawaida wanayotangamana nayo kwa shughuli zao za kijamii. Dhana hii huwafanya wanafunzi kujua kuwa njia mwafaka ya kuifahamu matini husika ni kuingiliana moja kwa moja na matini hayo kama anavyosisitiza Jean Piaget katika Nadharia yake ya Maendeleo ya Utambuzi (1896-1980).




Kielelezo cha 3:Nyenzo za kutazamwa na kusikilizwa

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

## MUHTASARI

Madhumuni ya makala haya yalikuwa kubaini aina ya nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari katika Kaunti ya Kakamega nchini Kenya kwa kuangazia madarasa ya mwanzo. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Maendeleo ya Kiutambuzi ya Jean Piaget Utafiti huu ulitumia muundo wa usoroveya elezi. Idadi lengwa ya utafiti huu ni walimu wa somo la Kiswahili pamoja na wanafunzi wa madarasa ya mwanzo katika shule za sekondari katika Kaunti ndogo ya kati ya Kakamega. Mtafiti alitumia mbinu za usampulishaji za kinasibu na kimakusudi kuteua sampuli ya kutumiwa ambayo ilikuwa theluthi moja ya idadi lengwa. Walimu ishirini na tano (25) ambao ni theluthi moja ya walimu wote wanaofundisha Kiswahili katika madarasa ya mwanzo katika shule za sekondari Kaunti ndogo ya kati ya Kakamega na wanafunzi mia mbili hamsini (250) walishirikishwa na data kukusanywa kwa kutumia miongozo ya uchunzaji, hojaji, mahojiano na uchanganuzi wa nyaraka. Data ziliwasilishwa kwa kutumia maelezo, vielelezo na viwango vya kiasilimia. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kwamba, walimu wanatumia aina tatu za nyenzo: nyenzo za kutazamwa, nyenzo za kusikilizwa na nyenzo za kutazamwa na kusikilizwa katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili lakini hawatilii mkazo nyenzo zinazotokana mifumo ya kijamii katika kufundisha Fasihi Simulizi ya Kiswahili licha ya kuwepo.

## MAREJEO

Aras G. (2012). *Teaching writing through non library formats in Departments of English and literature*. Fronters of language & Teaching, 132-138

Bennaars, G. A, Otiende, J. E. & Boisvert, R. (1994*). Theory and Practice of Education.* Nairobi: East African.

Chesaina, C. (2007). *The Role and significance of Oral Literature in Social and Psychological Development of Children*. Nairobi: Nairobi University Press.

Clark, L. H., & Starr, S. L. (1986). *Secondary and Middle School Teaching Methods.* New York: Macmillan.

Creswell, J. W. (2006). *Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Research Approaches*. Thousand Oaks, CA: Sage.

Cross, G. P. (1974). *The Psychology of Learning.* Paris*:* Pergamon Press.

Donhardt, G. L. (1984). Microcomputers in education: Elements of a computer-based curriculum. *Educational Technology*, *24*(4), 30-32.

Dorr, A. (1984). *Television and Children.* Newbury Park*:* Calif Educational Publishers.

Farrant, J. S. (1980). *Principals and Practice of Education*. Essex England: Longman.

Gagne (2006). *The Condition of Learning.* New York: Holt Rinehart and Winston.

Gathumbi, A. W., & Ssebbunga, C. M. (2005). *Principles and Techniques in language Teaching; A Text for Teacher Educators. Teachers and pre-service Teachers,* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Henson, K. (1987). *Teaching Secondary and Middle Schools*. New York: Longman

KIE (2002). *Secondary School Syllabus*, Vol. 1. Nairobi: K.I.E.

KIE (2006). *Secondary School Syllabus*, Vol. I. Nairobi: K.I.E.

Kothari, C. (2012). *Quantitative Techniqu*es. (Toleo 3). New Delhi. Vicas publishing House Limited.

Kothari, C. R. (2003). *Research methodology: Methods and techniques*. New Delhi: Vishwa

Luvisia, J. C. (2003). *A study of availability and use of instructional resources in teaching Kiswahili grammar in selected secondary schools of Bungoma District, Kenya*. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Moi.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/eajss.2.2.227

Macharia, S. N., & Wario, L. H. (1989). T*eaching Practices in Primary Schools*. London: Macmillan.

Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (2003). *Research Methods Quantitative and Qualitative Approache*s. Nairobi: Acts Press.

Mugenda, O. M., & Mugenda, A. G. (2006). *Qualitative and Quantitative Approaches*. Nairobi: Acts press.

Musau, P., & Chacha, L, (2001). *Mbinu za Kufundisha Kiswahili*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mwakyembe, G. R. (1982). *Misingi ya Ualimu*. Dar es Salaam: General Publishers Ltd.

Ogulla, P. A. (2002). *Research Methods*. Nairobi: Catholic University of Eastern Africa.

Okwalo, P. O. (2012). *Matumizi ya Nyenzo katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika shule za sekondari Wilayani Mumias na Matungu*. Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Omstein, C. A. (1990). *Strategies for Teaching*. New York: Harper Collins.

Pappert, S. (1987). *Computer Criticism Vs Technocentric Thinking*.

Peil, M. (2002). *Social Science Research Methods. A Handbook for Africa*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Postman, N. (1979). *Teaching as A Counselling Activity*. New York: Delacorte. Prakashan.

Quist, D. (2000). *Primary Teaching methods*. Oxford UK: Macmillan.

Robinson, A. (1980), *Principals and Practices of Teaching*. London: George Allenand Unwin.

Shitohi, E. (1992).*"An Investigation into The Use of the Radio Component in Training Inservice Primary Teachers"*: A project Report Submitted in Partial Fulfilment of the Requirements for the Degree of M.Ed Kenyatta University (unpublished).

Sifuna, D. N. (1996). *Short Essays on Education in Kenya*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Singleton, R. A. (1993). Approaches to Social Research. New York: O. U. P.